# UTAWALA BORA NA UTAWALA WA SHERIA

## 1. Utangulizi

Toleo la tatu la Darubini ya Dira ya Maendeleo ya Taifa (DDMT) linaelezea utekelezaji wa nguzo ya tatu ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ambayo inalenga kuimarisha uongozi bora na utawala wa sheria nchini, ili kujenga uwezo wa Watanzania wa kuwafanya viongozi na watumishi wa umma kuongeza ufanisi katika utendaji - kazi na uwajibikaji. Uongozi bora na utawala wa sheria ni vichocheo muhimu katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii kupitia mifumo wa uwajibishwaji kwa wavunjaji wa sheria za kazi na utoaji wa motisha kwa wafanyakazi bora ili kuhamasisha ubunifu, ustadi, uvumbuzi na kuongeza ubora katika utoaji wa huduma kwa umma.

## 2. Utekelezaji wa nguzo ya tatu ya ya Dira ya Maendeleo ya Taifa

Kulingana na Dira 2025, jamii itakuwa na utawala bora na utawala wa sheria kama itakuwa na sifa nne zifuatazo: (i) yenye maadili mema na kuthamini utamaduni (ii) yenye uadilifu na kuheshimu utawala wa sheria (iii) isiyokuwa na rushwa na maovu mengine (iv) iliyoelimika na inayojiamini, inayojifunza kutokana na uzoefu wake na wa wengine, na yenye kumiliki na kubaini ajenda za maendeleo. Ili kuwa na sifa hizi Serikali iliweka mikakati mbalimbali kama ifuatavyo:

### *2.1 Kujenga jamii yenye maadili mema na kuthamini utamaduni*

#### *2.1.1 Maadili mema*

Neno maadili linatafsiriwa kama mwenendo mwema unaokubaliwa na jamii fulani kuwa sehemu ya maisha yao. Serikali ya Tanzania inaendelea kujenga utumishi wa umma wenye maadili mema kwa kuwa na viongozi waadilifu, wanaofuata maadili ya kazi zao katika kutekeleza majukumu yao. Aidha, viongozi wa umma wakiwa na dhamira timilifu juu ya uadilifu, ni rahisi kwa wananchi kujifunza na kuiga maadili mema kutoka kwao, kwa vile kauli na matendo yao yanatoa mfano mwema katika kuwaelekeza wananchi kuwa waadilifu pia.

Kwa kutambua umuhimu wa kujenga jamii yenye maadili mema Tanzania, Serikali ilianzisha Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi na Watumishi wa Umma ili kufuatilia maadili na mwenendo wa viongozi wa umma. Katika kufanikisha jambo hilo, Sekretarieti ya Maadili inasimamia utekelezaji wa sheria ya maadili ya viongozi wa umma, namba 13 ya mwaka 1995, inayowataka viongozi na wanasiasa kutoa tamko rasmi kuhusu mali na madeni yao baada ya uteuzi, kila mwisho wa mwaka na baada ya kuacha wadhifa. Kisha taarifa hizo kufanyiwa uhakiki kama zipo sahihi ili kuwawajibisha viongozi wanaotumia madaraka yao kulimbikiza mali pasipo uhalali. Takwimu za urudishaji fomu za tamko la mali kwa viongozi wa umma na viongozi wa kisiasa zinaonyesha kuwa kati ya mwaka 2010/11 na 2013/14 namba ya viongozi waliojaza na kurejesha fomu za tamko imeongezeka zaidi ya mara mbili; kutoka viongozi 3,770 mpaka viongozi 8,400 kwa mwaka.

Hili ongezeko lilitokana na hatua ya Serikali ya mwaka 2011 ya kuanzisha Baraza la Maadili ya Utumishi wa Umma ili kusikiliza malalamiko ya ukiukwaji wa maadili ya viongozi wa umma kama yanavyowasilishwa na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi. Ukiukwaji wa maadili ya utumishi wa umma unajumuisha matumizi mabaya ya madaraka na kushindwa kuwasilisha tamko la mali za viongozi. Wakati mwaka 2011, Baraza lilisikiliza jumla ya malalamiko 40, ambapo jumla ya viongozi 23 walikutwa na hatia na waliwajibishwa, mwaka 2013, Baraza lilipokea malalamiko 9 tu. Vilevile, Serikali ilianzisha Kamati za Uadilifu katika ofisi mbalimbali za serikali ikijumuisha wizara, idara, wakala zinazojitegemea, halmashauri za miji, majiji na wilaya, ili kujenga nidhamu na uwajibikaji wa watumishi kwa umma. Jarida la Sekretariati ya Maadili, toleo la tatu (Februari 2013) liliandika kuwa Serikali ilikuwa imeanzisha kamati 260 za uadilifu katika ofisi mbalimbali za Serikali.

Katika kuboresha uwajibikaji katika matumizi ya fedha, Serikali za mitaa hulazimika kubandika kwenye mbao za matangazo taarifa za bajeti, ikiwa ni mapato na matumizi, ili zisomwe na watu wote. Taarifa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Serikali za Mitaa kuhusu mchanganuo wa bajeti inaonyesha kuwa asilimia 95 ya Serikali za mitaa ziliweka taarifa zao za miradi na fedha kwenye mbao za matangazo kwa mwaka 2007/08, wakati mwaka 2012/13 zilipungua na kuwa asilimia 86, ingawa idadi hii ilizidi malengo ya MKUKUTA 2 ambayo ni asilimia 80 ya Serikali za mitaa, ifikapo mwaka 2015.

Udhibiti wa matumizi ya fedha katika mamlaka za Serikali za mitaa hufanyika pia kupitia ukaguzi ambao hufanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kila mwaka. Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zinaonyesha kuwa idadi ya Halmashauri zilizopata hati safi za ukaguzi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliongezeka toka Halmashauri 66 au asilimia 49 ya halmashauri 133, mwaka 2009/10, na kufikia Halmashauri 104 au asilimia 78 ya Halmashauri 134 mnamo mwaka 2011/12.. Hili ongezeko limetokana na jitihada mbalimbali za udhibiti na usimamizi wa fedha zinazoendelea ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa Mfumo Maalum wa Usimamizi wa Fedha, ili kuhakikisha utunzaji mzuri wa kumbukumbu za mahesabu na utoaji wa taarifa sahihi za mapato na matumizi ya mikoa na halmashauri zake. Aidha, mafunzo ya utunzaji mahesabu yametolewa kwa maofisa wanaohusika katika ngazi mbalimbali za Serikali.

#### *2.1.2 Kutathmini utamaduni*

Sekta ya Maendeleo ya Utamaduni nchini bado inakabiliana na changamoto kubwa ya kuendelea kumomonyoka kwa maadili, hasa miongoni mwa vijana kutokana na athari za utandawazi. Serikali ya Tanzania, kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni, na Michezo, imeendelea kuenzi na kuhifadhi utamaduni, mila na desturi za Watanzania. Juhudi hizo zinaonekana kupitia uimarishwaji wa lugha ya Kiswahili kama kielelezo cha utamaduni wa Mtanzania. Wizara hiyo, ikishirikiana na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo husimamia na kuendesha Tamasha la Sanaa na Utamaduni wa Mtanzania ambalo limekuwa likifanyika kila mwaka, mwishoni mwa mwezi Septemba tangu mwaka 1981.

Katika Tamasha la 32 la Sanaa na Utamaduni lililofanyika mwaka 2013, jumla ya vikundi 38 kutoka nchini na vikundi vinne kutoka nje ya nchi vilishiriki. Vilevile, Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) limekuwa likiandaa na kurusha kila mwaka jumla ya vipindi 52 vya 'Lugha ya Taifa' kupitia kituo cha Redio TBC Taifa, vipindi 52 vya 'Kumepambazuka' kupitia Radio One na vipindi 52 vya 'Ulimwengu wa Kiswahili' kupitia Televisheni ya TBC 1. Vipindi hivyo vinalenga kuwahabarisha Watanzania juu ya umuhimu wa lugha ya kiswahili na matumizi sahihi ya lugha hiyo. Pia, Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni, na Michezo huandaa na kurusha kipindi cha 'Maadili ya Mtanzania' ambacho hurushwa kwenye kituo chaRredio TBC Taifa kila siku ya Alhamisi, kikilenga kuelimisha jamii, hususan vijana ili waenzi na kuthamini mila na desturi za Kitanzania.

Ili kujenga jamii inayothamini utamaduni kama ilivyoelekezwa kwenye Dira 2025, Serikali imeendelea kuweka mkazo katika kuhakikisha watumishi wa umma wanavaa mavazi ya heshima hasa wawapo katika sehemu za kazi. Hivyo, Serikali kupitia Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ilitoa Waraka Namba 3 wa mwaka 2007, unaotoa mwongozo wa mavazi ya heshima kwa mtumishi wa umma, ambayo yanazingatia mila na desturi za taifa letu.

### *2.2 Uadilifu na Kuheshimu utawala wa sheria*

Kwenye harakati za kuchochea maendeleo ya Watanzania, Serikali imeweka umuhimu katika kujenga uadilifu wa viongozi na watumishi wa umma katika utendaji kazi. Ni dhahiri kuwa viongozi wa umma wakiwa na uadilifu, wataonyesha mfano mzuri utakaowahamasisha wananchi kujifunza na kuiga kutoka kwao, na hivyo kujenga na kukuza uadilifu katika taifa zima.

Juhudi mbalimbali zinafanyika ili kuelimisha umma juu ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Taasisi inayosimamia sheria hiyo ni Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi na Watumishi wa Umma. Taasisi hiyo huwa inarusha vipindi vya redio TBC Taifa kila siku ya Jumanne jioni, ambapo wananchi wengi wanapata fursa ya kujifunza na kutoa maoni yao kwa njia ya simu, kuhusu maadili ya viongozi na watumishi wa umma.

Vilevile, ili kuimarisha uadilifu katika utendaji kazi, mafunzo mbalimbali yamekuwa yakitolewa kwa viongozi na watumishi wa umma, ili kuwawezesha kusimamia na kuimarisha maadili na uwajibikaji. Taarifa ya mafunzo ya maadili kwa viongozi na watumishi wa umma inaonyesha kuwa idadi ya viongozi na watumishi wa umma walioshiriki mafunzo ilifikia 2, 703 kuanzia mwaka 2010 hadi 2013.

Hata hivyo, pamoja na juhudi ambazo zimefanyika, changamoto kubwa katika utumishi wa umma ni kuwepo kwa baadhi ya viongozi wanaotumia vibaya madaraka yao kwa kujilimbikizia mali isivyo halali. Katika kuheshimu utawala wa sheria, changamoto kubwa ni suala la raia kujichukulia sheria mkononi unapotokea uhalifu kwa kuwaadhibu wahalifu bila kufuata taratibu zinazotakiwa ama kuwafikisha au kutoa taarifa katika vyombo husika. Tarifa kutoka Jeshi la Polisi zinaonyesha kuwa mauaji yaliyotokana na kujichukulia sheria mikononi yamekuwa yakiongezeka kila mwaka kutoka mauaji 503 mwaka 2006 hadi kufikia mauaji 716 mwaka 2012. Moja ya Sababu kuu ya tabia hii ya kujichukulia sheria mkononi ni kile kinachosemekana kuwa ni hasira kali ya wananchi kila uhalifu unapotokea.

### 2.3 *Kutokuwepo rushwa na maovu mengine*

Ili kuhakikisha rushwa inatokomezwa nchini, Serikali iliunda Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kama chombo huru kinachoongozwa na Sheria namba 11 ya mwaka 2007 ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Taasisi hiyo imeonyesha mafanikio katika utendaji ambapo kiasi cha fedha shilingi za Kitanzania bilioni 39.93 zilizookolewa. Aidha kesi mpya za rushwa 1,175 zilizofunguliwa, 2,193 zilizopelekwa mahakamani na watuhumiwa 276 walipatikana na hatia.

Vilevile, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikiendesha misako na operesheni mbali mbali ili kudhibiti maovu mengine, kama vile biashara za madawa ya kulevya na ujambazi. Taarifa kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani zinaonyesha kuwa mwaka 2011 watuhumiwa 1,064 walikamatwa kwa kosa la kukutwa na zaidi ya kilo 22,000 za madawa ya kulevya. Vilevile, jumla ya ekari 309 za mashamba ya bangi ziliteketezwa katika Mikoa ya Tanga, Tabora na Tarime. Kwa mwaka 2013, ushirikiano kati ya wananchi uliliwezesha Jeshi la Polisi kuwakamata watuhumiwa 7,276 wakiwa na jumla ya kilo 31, 737.3 za dawa za kulevya. Aidha, jumla ya ekari 211 za mashamba ya bangi ziliteketezwa katika Kanda Maalum ya Kipolisi ya Tarime/Rorya na Mkoani Tanga. Vilevile, wananchi wengi wamekuwa na mwamko wa kujifunza kuhusu uimarishwaji wa ulinzi na kushirikiana na Jeshi la Polisi, ili kukabiliana na tatizo la uhalifu nchini. Takwimu za Jeshi la Polisi zinaonyesha ongezeko la idadi ya vikundi vya ulinzi shirikishi kutoka vikundi 2,832 mwaka 2011 hadi vikundi 4,850 mwaka 2013.

Vijana wengi wameonyesha ari ya kujifunza kupambana na maovu mbalimbali katika jamii, kwa kujiunga katika klabu mbalimbali zinazoanzishwa shuleni. Katika mwaka 2013, vijana zaidi ya 330 kutoka shule za sekondari zilizopo mkoani Dar es Salaam walishiriki katika kongamano kubwa la klabu za wapinga rushwa, ambapo vijana hao walielimishana kuhusu mapambano dhidi ya rushwa.

### 2.4 *Jamii iliyoelimika na inayojiamini, inayojifunza kutokana na uzoefu wake na wa wengine na yenye kumiliki na kubaini ajenda za maendeleo yake*

Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa taifa linakuwa na watu walioelimika, kupitia utolewaji wa fursa sawa katika elimu. Kutokana na juhudi zilizofanyika, idadi ya wanafunzi waliopo kwenye shule za msingi na sekondari imekuwa ikiongezeka, kuashiria mwamko wa wananchi katika kutambua umuhimu wa elimu. Takwimu kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi zinaonyesha kuwa idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika shule za msingi nchini iliongezeka toka 897,569 mwaka 2000 na kufikia 1,404,998 mwaka 2012. Katika kipindi hicho, idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika shule za sekondari iliongezeka toka 261,896 na kufikia 1,884,272. Pia Serikali imeongeza ushirikiano na sekta ya watu binafsi katika kutoa elimu katika ngazi zote idadi ya shule nchini. Katika ngazi ya secondary idadi ya shule za binafsi imeongezeka kutoka 649 mwaka 2003 hadi shule 3,500 mwaka 2012.

Pia, juhudi nyingine inayofanywa na Serikali ili kujenga jamii iliyoelimika ni kuongeza idadi ya vyuo vya ufundi ili kuwaongezea wanachi ujuzi wa kazi mbalimbali. Idadi ya vyuo hivyo imeongezeka kutoka vyuo 168 mwaka 2007, hadi vyuo 750 mwaka 2011.

Pamoja na ongezeko la idadi ya wanafunzi katika shule za msingi, sekondari na vyuoni, bado Serikali inakabiliwa na changamoto ya kutokuwepo ubora unaopaswa katika elimu inayotolewa katika shule hizo pamoja na uhaba wa vifaa vya kufundishia. Hivyo, juhudi zaidi zinahitajika ili kuongeza idadi ya walimu, vitabu na vifaa vingine vya kufundishia na kuwahamasisha walimu waliopo kwa ajili ya kutoa elimu iliyo bora.


**Economic and Social Research Foundation (ESRF)**
P.O. Box 31226, Dar es Salaam, Tanzania.
Phone: (+255) 754 780 133, (+255) 777 790 133,
(+255) 782 780 133 • Fax: (+255 22) 2760062
E-mail: esrf@esrf.or.tz • Website: www.esrf.or.tz


# DARUBINI YA DIRA YA MAENDELEO YA TAIFA 2025

## UTAWALA BORA NA UTAWALA WA SHERIA







Toleo la TATU